## Josia Asangalwisye Mwakalinga, (1935–1984)

Josia Asangalwisye Mwakalinga alikuwa mchungaji wa mstari wa mbele, mwenye kupanda makanisa, mfundishaji, mhazini, na msimamizi wa kazi katika Tanzania.

### Maisha ya Awali

Josia Asangalwisye Mwakalinga alizaliwa mwaka 1935 huko Lupando, Masoko Rungwe, Mbeya Tanzania. Wazazi wake wote wawili, Asangalwisye Mwakalinga na mkewe, walikuwa wazaliwa wa Masoko Mbeya. Wazazi hao hawakuwa waumini wa Kiadventista, bali ni mjomba wake, Tito Mwakalinga, aliyekuwa amepokea ujumbe wa Waadventista alipokuwa akiishi Mwanza. Aliacha kazi yake ya uanajeshi na kurudi nyumbani Mbeya ambako alishiriki ujumbe huo na Josia Mwakalinga, naye akaukubali.

Josia Mwakalinga alikuwa mzaliwa wa kwanza kati ya watoto sita wa wazazi wake. Akiwa mzaliwa wa kwanza, aliishi maisha ya kielelezo yaliyojenga msingi thabiti wa kumwamini Mungu kwa wanafamilia wengine.

### Elimu

Josia Asangalwisye Mwakalinga alipata elimu yake ya msingi katika Shule ya Msingi ya Bunyangomale, na Shule ya Kati ya Suji hadi darasa la nne. Pia alienda Ikizu kwa kozi ya ualimu kwa mwaka mmoja. Akiwa Ikizu, alichukua kozi ya uhasibu katika chuo hicho kwa muda wa miaka miwili, na kuimaliza mwaka wa 1956. Alifanya kazi kama mwalimu wa shule kwa miaka michache na kisha akaamua kuhudhuria Chuo cha Waadventista cha Bugema kwa kozi ya miaka miwili ya uchungaji, ambayo iliendeshwa kuanzia 1964 hadi 1966. Mafanikio yake ya kielimu yaliwapa changamoto wahudumu vijana wa siku zake, kama vile Mchungaji L. Mwamakamba, na Mchungaji Mwambalangania, ambao walihimizwa kuendelea na masomo kutokana na msukumo wake. Wakati huo, Kanisa la Afrika lilikuwa na Waafrika wachache wenye shahada za elimu.

### Ndoa na Familia

Mchungaji Josia Mwakalinga alimuoa Essah Hamsole Mwanyilu mnamo Februari 24, 1960, na walitumika pamoja kama timu katika huduma. Mungu aliwabariki na watoto saba, mmoja wa kiume na sita wasichana: Albetina, Tukumbuke, Agness, Asangalwisye, Tupokigwe, Bupe, na Iganile. Watoto wanne kati ya hao bado wanaishi, kama ilivyo kwa mama yao, Essah Mwakalinga. Binti yao Agnes na mumewe wanafanya kazi katika Konferensi ya Mashariki-Kati mwa Tanzania kama katibu muhtasi wa ofisi za makao makuu ya Konferensi na mkurugenzi wa vijana, mtawalia.

**Uchungaji**

Mchungaji Josia Asangalwisye Mwakalinga alijiunga na huduma hiyo ya kichungaji baada ya kupokea mwito mwaka 1960 wa kufanya kazi kama mweka hazina katika eneo jipya la Busegwe, ambako Kanisa lilimtuma pamoja na mmishonari Mzungu kwenda kufungua kazi huko. Alifanya kazi kama katibu/mweka hazina wa Shamba la Bupandagila kuanzia 1961 hadi 1962, kisha akaenda shule. Kuanzia 1967 hadi 1971 alifanya kazi Bupandagila kama mkurugenzi wa idara ya vijana. Kuanzia 1972 hadi 1975, alikuwa mkurugenzi wa vijana huko Morogoro katika Tanzania General Field. Kuanzia 1975 hadi 1976 alifanya kazi kama mchungaji aliye mstari wa mbele. Kuanzia 1976 hadi 1977, Mchungaji Josia Asangalwisye alikuwa mkurugenzi wa idara ya uchapishaji. Kuanzia 1977 hadi 1981 alikwenda Dar es Salaam kama mchungaji aliye mstari wa mbele. Kuanzia 1981 hadi 1984 alifanya kazi huko Dodoma kama mchungaji aliye mstari wa mbele. Kutoka Dodoma alikwenda Mbeya kwa nafasi hiyo hiyo.

**Miaka ya Baadaye na Urithi Aliotuachia**

Mnamo 1972, akiwa mchungaji wa mstari wa mbele huko Dodoma, Mchungaji Mwakalinga aliugua homa ya ini. Kanisa na familia yake walimpeleka katika hospitali kama vile Tabora Hospital, Lugalo Hospital-Dar es Salaam, Dodoma Hospital, na Mbeya na Makandana Hospital; lakini hawakufanikiwa kuokoa maisha yake. Alifariki mwaka 1984 na kuzikwa Bunyangomale-Masoko, Tukuyu Mbeya.

Mchungaji Josiah Mwakalinga anakumbukwa kwa kujitoa katika uinjilisti na uanzishaji wa makanisa.